OMBA KWA JINA LANGU

Mwandishi: G. I. Harlow

EVERYDAY PUBLICATIONS INC.
310 Killaly St. W.
Port Colborne ON L3K 6A6
Canada

Copyright © 1976 Everyday Publications Inc.

ISBN 0-88873-171

Imprimé au Canada
Copyright © 1976 Everyday Publications Inc.

"OMBA KWA JINA LANGU"

"Na mukiomba lo lote kwa jina langu, nitalifanya, Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Kama mukiomba neno gani kwa jina langu nitalifanya." [Yoane 14:13-14]

Nani alisema maneno haya matamu katika Yoane 14:13-14? Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Alikuwa akifundisha wanafunzi juu ya maombi, na pamoja na agizo hili kuomba kwa jina lake aliwapa ahadi ya ajabu: alisema atafanya neno lo lote ambalo wataomba, ili Mungu Baba atukuzwe ndani ya Mwana wake.

Maombi ni nini? Ni kuomba Mungu Baba kwa jina la Mwana wake, ndiye Bwana Yesu Kristo, kutupa sisi vitu tunavyohitaji, na kuweka mbele yake maneno mbalimbali mengi tunayotaka afanye kwa sisi na kwa watu wengine.

Ndani ya kitabu hiki utaona kwa ufupi zaidi ya maneno ambayo Neno la Mungu linatufundisha juu ya maombi. Roho Mtakatifu tu anaweza kukufundisha kuomba, kama ukimpa njia kufanya hivi. Lakini sharti ujue maneno ambayo Mungu anatufundisha juu ya maombi ndani ya Kitabu chake.

Kitabu hiki kina sehemu au sura 30. Utasaidiwa zaidi kama ukisoma sehemu moja kila siku ukiangalia mashairi yote yanayotajwa ndani ya Biblia yako mwenyewe. Kwa njia hii utaweza kujifunza maneno yote ndani ya kitabu hiki katika muda wa mwezi mmoja.

Tunaomba Mungu aweze kutumika na kitabu hiki kidogo kuongeza hamu yetu kusemezana na kushiriki na Mungu kwa njia ya maombi.

"Bwana, utufundishe sisi kuomba"

(Luka 11:1)

Copyright © 1976 Everyday Publications Inc.

Maulizo juu ya Maombi

Watu wanafazaika juu ya maneno mengi wakati wanapowaza juu ya maombi. Tunataja mengine ya maneno haya hapa:

Ona mafundisho juu ya ulizo hili kwa *ukurasa*

1. Maombi ni nini? 6
2. Namna gani mimi, mwenye zambi, ninaweza kukaribia Mungu mtakatifu kwa maombi? 7
3. Kwa nini inanipasa kuomba Mungu? 8
4. Inanipasa kuomba Mungu namna gani? 9
5. Inanipasa kutumia masemo ya namna gani wakati ninaposema na Mungu? 9
6. Msiyeamini anaweza kuomba Mungu? 10
7. Inanipasa kuomba Mungu kwa maneno gani? 11
8. Kuna maneno mengine ambayo Biblia inaniagiza kuomba juu yao? 12
9. Maana ya kuomba kwa "watu wote wa Mungu" ni nini? 13
10. Maana ya kuomba kwa "watu wote" ni nini? 14
11. Ninaweza kuomba Bwana juu ya neno lo lote kwa wakati wo wote? 15
12. Mungu anasikia kweli wakati ninapoomba kwake? 16

13,14 Mungu atajibu maombi yangu? 16,17

15. Kuna neno linaloweza kuzuiza Mungu asijibu maombi yangu? 18
16. Mungu atajibu maombi yangu kila mara namna ninavyotaka? 19

Copyright © 1976 Everyday Publications Inc.

ukurasa

17. Maombi yangu mengi yanaweza kuchokeza Mungu? 20
18. Maana ya maombi ni kuomba tu kupewa vitu tunavyotaka? 21
19. Inanipasa kuomba mara ngapi? 22
20. Inanipasa kuomba mara ngapi kwa neno fulani moja? 22
21. Mara nyingine Mungu anafanya neno ninaloomba kama si mapenzi yake? 23
22. Inanipasa kwenda pahali gani kwa maombi? 24
23. Inanipasa kushinda saa ngapi kwa maombi? 25
24,25 Inanipasa kukaa namna gani saa ninapoomba? 26,27
26. Ni vizuri kwa mimi kuomba wakati mimi ni peke yangu tu, au pamoja na watu wengine vilevile? 28
27. Inapasa mtu kuomba namna gani kwa kusanyiko la Wakristo? 28
28. Maombi yatageuza maisha yangu kwa njia yo yote? 29
29. Maombi yana faida gani kwa kazi ya Bwana? 30
30. Namna gani ninaweza kujifunza kuomba? 31

Una maulizo mengine vilevile? Vizuri uyaandike juu ya karatasi. Labda utapata majibu kwa maulizo yale ndani ya kitabu hiki vilevile.

Copyright © 1976 Everyday Publications Inc.

~1 ~
MAOMBI NI NINI?

Mtu anaomba wakati anaposemezana na Mungu juu ya neno lo lote, maneno ambayo yanamfazaisha, mahitaji yake ya mwili au ya roho, maneno ambayo yanamfurahisha au kumhuzunisha. Ni kuomba Mungu kukusaidia, kukuongoza, kukupa nguvu, kuokoa wapenzi wako na ndugu zako, na maneno mengi mengine usiyoweza kufanya wewe mwenyewe. Ni kushukuru Mungu vilevile kwa maneno yote ambayo anakwisha kukufanyia. Soma Wafilipi 4:6.

Kwa mfano waza juu ya watu hawa wa Agano la Kale walioomba kwa maneno mbalimbali:

1. Yakobo aliomba Mungu ku**mlinda** ili ndugu yake Esau asimwumize (Mwanzo 32:9-11).
2. Gideoni aliomba Bwana kumwongoza kwa njia ya ngozi (Waamuzi 6:39).
3. Hana aliomba Mungu **kumpa mwana** (1 Samweli 1:9-11).
4. Samweli aliomba wakati aliposihi Mungu kushinda Wafilistini (1 Samweli 7:9-10).
5. Mfalme Solomono aliomba Mungu **kumpa akili** ili aweze kutawala Waisraeli vizuri (1 Wafalme 3:5-9).

~ 2 ~

NAMNA GANI MIMI, MWENYE ZAMBI, NINAWEZA KUKARIBIA MUNGU MTAKATIFU KWA MAOMBI?

Ndiyo, Mungu ni mtakatifu na anachukia zambi. Hawezi kutazama mabaya bila kukasirika (Habakuki 1:13) na hawezi kukubali wenye zambi kusimama mbele yake na zambi zao zote.

Na kweli **watu wote** ni wenye zambi (Waroma 3:23), na hakuna mtu hata mmoja aliye mwenye haki (Waroma 3:10). Basi NAMNA GANI watu wenye zambi wanaweza kukaribia Mungu mtakatifu? Unauliza vizuri – na utapata jibu la kukushangaza.

Jibu ndilo hili: **kwa njia ya Kristo**. Mungu alituma Mwana wake wa pekee, Mwana mpendwa, hapa duniani kufa kwa wenye zambi. Kristo alibeba azabu ya Mungu kwa zambi zetu wakati alipokuwa juu ya msalaba (1 Petro 2:24), na kwa sababu alijitoa mwenyewe kama sadaka kwa zambi zetu sisi tunaweza kugeuka watu wa nyumba ya Mungu (Waefeso 2:19).

Kwa wakati wa sasa Bwana Yesu ni Kuhani Mkubwa wetu. Anatusimamia mbele ya Mungu na anatuombea wakati wote (Waebrania 7:25). Kwa sababu hii mwandishi wa barua kwa Waebrania anatuagiza kukaribia kiti cha neema pasipo woga, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji (Waebrania 4:16). Hivi tunaweza kuja kupata neema kwa njia ya maombi.

~ 3 ~

KWA NINI inanipasa kuomba Mungu?

Ninaamini ya kwamba Mungu ananipenda na ya kwamba anaongoza maneno yote ambayo yananipata. Ninaamini anajua mahitaji yangu na anatuma kwangu maneno yale tu yaliyo kwa baraka yangu. Basi kwa nini anataka mimi ***kuomba*** *kwa maneno haya?*

Unataka kujua kwa nini inakupasa kuomba? Ni kwa sababu:

1. **Mungu ana*taka* ufanye hivi.** Mungu ni kama baba ya dunia anayejua mahitaji ya mtoto wake lakini anayetaka mtoto kumwomba kwa vitu vile anavyotaka. Mungu anataka sisi watoto wake kufika mbele yake kwa maombi kwa sababu anatupenda na anapenda kusikia sauti zetu. Anataka tumtegemee kwa mahitaji yetu yote kwa sababu anajua neno hili litatusaidia kukaa karibu naye.

2. **Mungu anaku*agiza* kufanya hivi**. Neno hili ni neno kubwa sana. Tunaagizwa kuomba siku zote, pasipo kuchoka (Luka 18:1). Soma vilevile Luka 21:36; Waefeso 6:18 na 1 Watesalonika 5:17.

~ 4 ~

Inanipasa kuomba Mungu NAMNA GANI?

1. Tumesema mbele ya kwamba Mungu ni mtakatifu na haifai tusahau neno hili kamwe wakati tunapoomba. Sharti tukumbuke ya kwamba yeye ndiye Mwumba wetu nasi tuliumbwa naye. Hivi yeye ni mkubwa kupita sisi na ingetupasa kufika mbele yake **na unyenyekevu na kumwonyeshea heshima wakati tunaposema naye**.

2. **Mungu anataka sisi kuomba na roho ya kweli, si na udanganyifu**. Haifai tuseme tu maneno fulani na kinywa na kuwaza maneno mengine rohoni (Zaburi 145:18). Ingetupasa kuomba juu ya maneno yetu wenyewe wakati sisi ni peke yetu pamoja na Mungu. Tukiomba juu ya maneno haya mbele ya watu wengi, labda watafikili sisi ni Wakristo wazuri sana. Haifai kuomba kwa kuonekana mbele ya watu. Soma maneno Bwana Yesu aliyosema juu ya neno hili katika Matayo 6:5-6.

~ 5 ~

Inanipasa kutumia MASEMO YA NAMNA GANI wakati ninaposema na Mungu?

Vizuri tumwambie tu waziwazi maneno tunayotaka yeye kujua na maneno tunayotaka ayafanye. Haifai tutumie maneno marefu, au maneno wenye elimu wanayotumika nayo, wala kuomba maombi marefu kama wapagano wanavyofanya wakati wanapoomba kwa miungu yao (Matayo 6:7).

Bwana Yesu alitupa sisi mfano mzuri sana wa namna gani anataka sisi kuomba. Soma Matayo 6:9-13 polepole na ona ya

kuwa ombi hili linajaa na heshima kwa Mungu na ya kwamba masemo Bwana Yesu aliyotumia si masemo ya elimu. Tutawaza juu ya mashairi haya tena nyuma.

~ 6 ~

MSIYEAMINI anaweza kuomba Mungu?

Zaidi ya wasioamini hawana hamu kuomba Mungu. Lakini mara nyingine Mungu anachokoza zamiri zao kwa njia ya kutuma taabu au hatari kwao na halafu wanalia kwake awasaidie. Wabaharia katika Yona 1:14 walifanya hivi. Mara nyingine watu namna hii wanaahidi Mungu ya kwamba watageuka wafuata wake na kumtumikia kama akiwaponyesha toka taabu yao. Mungu anasikia na kujibu maombi ya namna hii? Bila shaka anayasikia na mara nyingine anayajibu vilevile.

Kuna ombi moja mtu asiyeokolewa kwanza analoweza kuomba na bila shaka Mungu atajibu ombi hili na furaha. Ni ombi ambalo mtoza kodi aliomba hekaluni (Luka 18:13). Mtu huyu alijua ya kwamba alikuwa mwenye zambi na hakustahili kufika karibu na Mungu. Alikuwa na huzuni juu ya zambi zake na alichoka nazo, hivi aliomba Mungu na unyenyekevu kabisa kumrehemu na kumsamehe. Unafikili Mungu alijibu ombi lake? Kabisa! Ona shairi 14. Anafanya vivyo hivyo kwa kila mwenye zambi anayetubu na kufika kwake na unyenyekevu kwa kuomba usamehe. Ndiyo, na kuna furaha kubwa mbinguni juu ya kila mtu mwenye zambi anayetubu (Luka 15:7). Hili ndilo ombi la kwanza inalopasa kila mtu kuomba.

~ 7 ~

Inanipasa kuomba Mungu KWA MAMBO GANI?

Soma Luka 11:2-4 tena. Haya ndiyo masemo ya Bwana Yesu mwenyewe. Tunaagizwa kuomba

1. **kwa Mungu Baba kutukuzwa**. Kwa pahali pengine Bwana Yesu alisema ya kwamba atafanya neno lo lote tunaloomba kwa jina lake ili Baba Mungu atukuzwe ndani ya Mwana (Yoane 14:13).
2. **mapenzi na makusudi ya Mungu yafanyike duniani.** Tusaidie kutimiza maombi haya kwa njia ya kufanya mapenzi yake sisi wenyewe (Zaburi 40:8).
3. **Baba kutupa sisi vyakula tunavyohitaji kila siku.** Ameahidi kutupa sisi vitu vyote tunavyohitaji kama tukiweka ufalme wake na haki yake kwanza (Matayo 6:33).
4. **Baba kusamehe zambi zetu** – kama vile tukiwasamehe wale ambao walitukosea sisi. Bwana Yesu alituambia wazi kabisa katika Matayo 6:15 ya kwamba Mungu hatasamehe zambi zetu kama sisi tusiposamehe mabaya ambayo watu wengine walitutendea vilevile.

Ona ya kwamba ndani ya ombi hili **utukufu wa Mungu na mapenzi yake ni kwa pahali pa kwanza,** si mahitaji yetu na maneno yetu mengine.

~ 8 ~
Kuna maneno mengine ambayo Biblia inaniagiza kuomba juu yao?

Ndiyo, Biblia inatuagiza kuomba juu ya maneno mengine vilevile. Tunaagizwa kuomba:

1) **kwa wale ambao wanatutesa** (Matayo 5:44). Bwana Yesu alifanya hivi yeye mwenyewe (Luka 23:34), na mtumishi wake Stefano alifanya vivyo hivyo (Matendo 7:60). Ni nguvu kufanya neno hili lakini litatusaidia kushinda wakati tunapoteswa kwa sababu ya imani yetu.
2) **ili tusishindwe na majaribu** (Matayo 26:41). Bwana aliahidi ya kwamba hatutajaribiwa kupita kipimo chetu, lakini wakati tunapojaribiwa atatupa sisi nguvu kuvumilia na atafanya vile njia kwa sisi kuweza kutoka ndani ya majaribu yenyewe (1 Wakorinto 10:13).
3) **Bwana kutusaidia wakati tulipo na ugonjwa au taabu nyingine** (Yakobo 5:13). Bwana Yesu anatuhurumia katika uzaifu wetu, wa mwili, na wa roho vilevile (Waebrania 4:15), naye anatuombea siku zote mbele ya Mungu (Waebrania 7:25). Ni ajabu kabisa!
4) **kwa watawala walio na amri juu yetu** (1 Timoteo 2:1-2). Na pamoja na kuwaombea inatupasa kuwatii (Waroma 13:11) na kuwaheshimu.
5) **kwa wale wanaotumikia Bwana**. Paulo alisihi Wakristo tena na tena kumwombea (Waroma 15:30-31; Waefeso 6:19; 1 Watesalonika 5:25; 2 Watesalonika 3:1). Kila mtumishi wa Mungu anafahamu ya kwamba anapiga vita na adui yake Shetani na ya kwamba anahitaji sana maombi ya Wakristo. Unaweza kushiriki katika utumishi wake kwa Bwana, na zawabu yake, kwa njia ya kumwombea kila siku!

6) **ili Mungu, Bwana wa mavuno, aweze kutuma watumishi wengine** kukusanya mavuno yake (Matayo 9:38). Watu wengi zaidi wangeamini Bwana Yesu kama watu wengi zaidi wangekuwa tayari kuwapasha habari zake. Wale tu wanaweza kuomba ombi hili na roho ya kweli walio tayari kwenda wao wenyewe kama Bwana akitaka kuwafanya wavunaji katika shamba lake.

~ 9 ~

Maana ya kuomba kwa "WATAKATIFU WOTE" ni nini? [Waefeso 6:18]

Maana yake ni wazi tu – ni kuombea Wakristo wote!

1) **Ni watu wale wa jamaa yako walio katika Kristo.** Unataka walindwe katikati ya majaribu mengi ambayo yanawazunguka, na kukaa kufuata Bwana? Kama ni hivi, sharti uwaombee. Vizuri uombe Mungu vilevile kukupa mapendo na ufahamu na uvumilivu wakati unapokaa katikati yao ili uweze kuwasaidia vizuri.
2) **Ni rafiki zako Wakristo** na wale unaoshiriki nao kanisani na kwa kazi ya Mungu.
3) **Ni wazee wa kanisa lako**. Omba Mungu kuwapa akili nyingi na nguvu kwa kazi yao ya kuongoza na kusaidia Wakristo wengine na kuongoza maneno ya kanisa. Wakristo wote wakiombeana, hakutakuwa na wivu na magomvi na mabishano katikati yao. Ni kazi ya wazee kuchunga utaratibu.
4) **Ni watumishi wa Mungu** wanaotumia saa zao zote kwa kazi ya Bwana. Omba Mungu
   a) waweze kuwa wanyenyekevu na kutembea karibu sana naye;

b) abariki kazi wanayofanya kwaye;

c) aweze kuwapa vyote wanavyohitaji kwa njia ya roho, mwili, na mali. Unaweza kuongeza matunda yao kwa kazi ya Bwana kwa njia ya kuwaombea.

Kwa wakati wa sasa Bwana Yesu Kristo anatuombea sisi (Waebrania 7:25), na tuko karibu zaidi naye wakati tunapofanya kazi hii vilevile, ndiyo kuombea watu wake.

~ 10 ~

Maana ya KUOMBA KWA "WATU WOTE" ni nini? [1 Timoteo 2:1]

Ni kuomba kwa wasioamini ndani ya jamaa yako. Hakuna mtu mwingine ambaye atawaombea isipokuwa wewe! Ni kazi yako kabisa.

Ni kuombea vilevile wasioamini wanaokaa ndani ya nyumba kando ya nyumba yako, na wale unaotumika kazi pamoja nao au kukutana nao kwa njia mbalimbali. Omba Bwana:

1) kukupa akili wakati unapojaribu kuwapasha Habari Njema;

2) kuwasaidia kufahamu na kukubali ya kwamba wao ni wenye zambi, wapotevu;

3) kuwapa hamu kugeuka Wakristo kwa sababu wanaweza kuona Kristo ndani ya maisha yako;

4) kuwapa imani na kuwasaidia kupokea Bwana Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao wenyewe.

Kuomba kwa watu wote ni kuomba kwa milioni za watu katika dunia nzima wasiojua bado Habari Njema, ili waweze kuisikia na kuokolewa.

~ 11 ~

Ninaweza kuomba Bwana juu ya NENO LO LOTE kwa WAKATI WO WOTE?

Ndiyo; na zaidi ya ile tunaagizwa kuomba kwa kila wakati katika roho (Waefeso 6:18). Hata ukifanya maneno gani, inge-kupasa kuomba Bwana juu yao.

Unatembea ndani ya motokari? Omba Bwana kukulinda.

Wewe ni kwa pahali pa kazi? Omba Bwana kukusaidia kufanya kazi yako kwa utukufu wake.

Unavua mavazi au kupika vyakula au kufanya kazi nyingine nyumbani? Omba Bwana kukusaidia na kukupa fura-ha kwa kazi ya kuchunga bwana na watoto ambao Mungu alikupa.

Una watoto? Halafu inakupasa kuomba Bwana tena na tena kukupa saburi na ufahamu wakati unapojaribu kuwafundisha na kuwaongoza kutembea vizuri.

Omba Mungu wakati unapokwenda shambani au dukani, wakati unapofundisha watoto siku ya Bwana, wakati ulipo mgeni nyumbani mwa watu wengine au wakati unapopokea wageni nyumbani mwako. Ndiyo, omba kwa kila wakati.

~ 12 ~

Mungu ANASIKIA kweli wakati ninapoomba kwake?

Ndiyo, Mungu anatusikia wakati tunapoomba. Mwandishi wa Zaburi 4:3 alijua neno hili kabisa. Soma vilevile Zaburi 6:9 na 34:17. Nabii Mika alijua vilevile ya kwamba Mungu atamsikia (Mika 7:7). Yona alililia Bwana wakati alipokuwa katika taabu kubwa na Bwana alimsikia (Yona 2:2). Sharti usome mashairi haya ndani ya Biblia yako mwenyewe!

Lakini kuna neno moja litakalofunga masikio ya Mungu asisikie maombi yetu. Hatusikii wakati tunapofanya zambi na hatujakiri zambi hii bado (Isaya 59:2).

~ 13 ~

Mungu ATAJIBU maombi yangu?

Ndiyo, Mungu anakusikia, na zaidi ya ile ameahidi kujibu maombi yako. Soma mashairi yanayofuata polepole na kuwaza sana juu yao:

"Ombeni na mutapata" (Luka 11:9).

"Kama mukiomba lo lote kwa jina langu, nitalifanya" (Yoane 14:14).

"Kama mukikaa ndani yangu, na maneno yangu yanakaa ndani yenu, mutaomba neno gani munalotaka na mutafanyiziwa" (Yoane 15:7).

"Neno lo lote tunaloomba tunalipokea kwake kwa kuwa tunashika amri zake na kutenda maneno yanayopendeza machoni mwake" (1 Yoane 3:22).

"Vitu vyote mutakavyoomba katika maombi kama mukiamini, mutapokea" (Matayo 21:22).

Tushukuru Mungu wetu kwa ahadi hizi kubwa.

~ 14 ~

Wakati unapowaza juu ya mashairi haya utaona ya kwamba Mungu atajibu maombi yetu **kama**:

1) **tukiomba kwa jina la Bwana Yesu** (Yoane 14:14). Maana ya kuomba kwa jina lake ni nini? Ni kuomba kwa neno linalopatana na mapenzi yake. Ukifanya neno kwa jina la mtu mwingine, ni kusema unafanya neno yule mtu mwingine analotaka lifanywe. Hivi kuomba kwa jina la Kristo si kusema tu kwa mwisho wa maombi yako: "Ninaomba hivi kwa jina la Kristo," lakini ni kuomba kwa maneno yale yanayopatana na mapenzi yake.
2) **tukikaa ndani ya Kristo na maneno yake yakikaa ndani yetu** (Yoane 15:7). Maana yake nini? Kukaa ndani ya Kristo ni kuwa na upatano wa karibu sana naye. Maneno yake yanakaa ndani yetu wakati tunapoyasoma kila siku na kuwaza juu yao na kuongozwa nao kwa maneno tunayofanya na kusema. Maneno haya ni kweli ndani ya maisha yako? Halafu unataka maneno yale tu yanayopatana na mapenzi ya Mungu na unaweza kujua ya kwamba Mungu atajibu maombi yako wakati unapoomba kwa maneno haya.
3) **tukitii maagizo yake na kumpendeza ndani ya maisha yetu ya kila siku** (1 Yoane 3:22). Wakristo si chini ya sheria ya Musa sasa, lakini Bwana ametupa sisi maagizo mengi ndani ya Agano Jipya. Hivi ni lazima kwako kujua maneno yanayoandikwa ndani ya Agano Jipya ili uweze kujua kama Bwana akitaka wewe kufanya nini. Halafu sharti utii maagizo haya kama ukitaka Bwana kujibu maombi yako.
4) **tukiwa na imani**, maana yake kama tukiamini ya kwamba Bwana atatujibu (Matayo 21:22; Marko 11:24). Usifikili utapata kitu kutoka kwa Bwana kama ukiwa na shaka na kufikili kwamba labda hatajibu maombi yako (Yakobo 1:5-8). Usiombe namna waamini nyumbani mwa Maria walivyoomba wakati Petro alipokuwa gerezani. Waliomba

Mungu aweze kuondosha Petro toka gereza, lakini walisema kijakazi alikuwa na wazimu wakati alipowaambia ya kwamba Petro alisimama kwa mlango wa nyumba! Hawakuamini kabisa kabisa ya kwamba Mungu atajibu maombi yao! Soma Matendo 12:5-17.

Lakini Hana aliomba na imani kweli (ona 1 Samweli 1:1-18). Hana alikuwa na huzuni sana kwa sababu hakuwa na mtoto na alililia Bwana akimwomba kumpa mwana. Aliamini ya kwamba Mungu alikuwa amesikia maombi yake na atamjibu, na kwa sababu hii hakuwa na huzuni tena (sh.18).

~ 15 ~

KUNA NENO LINALOWEZA KUZUIZA MUNGU ASIJIBU MAOMBI YANGU?

Ndiyo, Biblia inaonyesha maneno machache yanayozuiza Mungu asijibu maombi yako mara nyingine. Ni maneno haya:

1. **Zambi usizokiri bado**. Tuliona neno hili mbele katika Isaya 59:1-2. Soma Zaburi 66:18 vilevile. Shairi hili ni shairi kubwa sana. Halafu inakupasa kufanya nini? Kukiri zambi yako, ili Mungu aweze kukusamehe na kukusafisha toka uzalimu wote (1 Yoane 1:9)!
2. **Udanganyifu wa moyo**. Mungu hatajibu maombi yako kama ukiomba kwa kuonekana mbele ya watu kusudi watu wafikili wewe ni Mkristo mzuri sana. Ona Matayo 6:5; 23:14; Marko 12:40.

3) **Ukosefu wa upatano katikati ya mume na mke**. Ingepasa mume na mke kukaa pamoja na salama, mume akipenda mke wake na kumchunga, na mke akitii mume wake. Isipokuwa hivi, Mungu hatajibu maombi yao (1 Petro 3:1-7).

4) **Makusudi mabaya**. Mara nyingine watu wanaomba Mungu kwa vitu wanavyotaka kwa faida au furaha yao wenyewe, si vitu visivyo kwa utukufu wa Mungu. Mungu hatajibu maombi haya (Yakobo 4:3).

~ 16 ~

Mungu atajibu maombi yangu kila mara NAMNA MIMI NINAVYOTAKA?

Sivyo. Mara nyingine atakupa kitu kizuri kupita au kufanya neno lingine. Inawezekana kwa wewe na mimi kuomba Mungu kwa kitu tunachofikili ni kitu kizuri, kitu kitakachotukuza Mungu, lakini Baba yetu anayejua maneno yote anajua kitu hiki kingeumiza kazi yake na kutuumiza sisi vilevile. Mungu Baba anapenda watoto wake, na hivi, kwa pahali pa kutupa sisi kitu tunachoomba anatupa kitu kilicho kizuri kupita, kitu kitakachokuwa baraka kwetu na kumtukuza yeye. Anajibu maombi yako – si namna wewe ulivyotaka, lakini kwa njia ya kukupa yaliyo bora kuliko yale uliyoomba!

Tunaweza kuona neno hili katika maisha ya Paulo. Paulo alikuwa na uzaifu mmoja mwilini ambao ulimtesa sana. Alifikili uzaifu huu ulimzuiza ndani ya kazi yake kwa Bwana, hivi aliomba Bwana mara tatu kuuondosha kwake. Lakini Bwana hakufanya neno Paulo aliloomba. Kwa pahali pa kuondosha uzaifu wake Mungu alijibu hivi: alimpa Paulo neema ya kutosha kubeba uzaifu na kuumia mwilini mwake na kumtukuza hata hivi. Halafu Paulo alianza kushukuru Mungu kwa uzaifu wake kwani alijuana na neema ya Mungu kupita mbele katika maisha yake kwa sababu ya neno hili (2 Wakorinto 12:7-9). Mara nyingi Mungu hatuondoshi katika taabu yetu wakati tunapomwomba kufanya hivi, lakini anatupa nguvu kumtukuza hata ndani ya taabu yenyewe. Tumshukuru katika mambo yo yote.

~ 17 ~

MAOMBI YANGU MENGI YANAWEZA KUCHOKEZA MUNGU?

Sivyo! Yakobo anatuambia ya kwamba tunakosa vitu tunavyotaka kwa sababu hatuombi Mungu kwa vitu hivi (Yakobo 4:2). Ni nguvu kwawe kuwa na saburi? Umeomba Mungu kukupa saburi? Hapana? Basi huwezi kutoa uzuru juu ya kukosa saburi kwani Bwana ni tayari kukupa saburi kama ukimwomba kufanya hivi.

Maneno yote yanawezekana na Mungu na hakuna neno linaloweza kumshinda (Mwanzo 18:14; Matayo 19:26), naye anatukuzwa wakati tunapoomba maneno makubwa kwake **tukiamini** ya kwamba atayafanya. Kama ukimwomba, atakuwezesha kufanya maneno usiyoweza kamwe kufanya kwa nguvu yako mwenyewe.

Waza juu ya Elia. Wakati Waisraeli walipokuwa wamekwenda mbali na Bwana na kuabudu mungu Bali, Elia aliomba Mungu kufanya neno lisilowezekana kwa watu (1 Wafalme 18:17-39). Yeye na watu wote wa Israeli walikusanyika kwa mlima wa Karmeli pamoja na manabii 400 wa Bali.

Basi Elia alitaka Mungu kufanya neno litakaloaminisha watu wote ya kuwa yeye ndiye Mungu wa kweli. Aliweka sadaka ya ngombe juu ya mazabahu na kumwanga mapipa kumi na mawili ya maji juu yake hata kuni na sadaka juu ya mazabahu zilioza kwa maji. Kisha aliomba Bwana kuonyesha ya kwamba yeye ndiye Bwana Mungu ili watu wa Israeli waweze kurudi kwake. Mungu alijibu maombi ya Elia kwa njia ya kutuma moto kuteketeza sadaka hata kama ilioza kwa maji. Halafu watu wote walishangaa kabisa, wakaanguka kifudifudi na kukiri ya kwamba Bwana ni Mungu wa pekee wa kweli. Hivi Mungu alitukuzwa kwa sababu Elia alikuwa na imani na alimwomba kufanya ajabu!

~ 18 ~

MAANAA YA MAOMBI NI KUPEWA TU VITU TUNAVYOTAKA?

Sivyo. Sehemu kubwa ya maombi ni sifa na mashukuru. Ndani ya Wafilipi 4:6 Paulo anatufundisha ya kwamba ingetupasa kuomba pamoja na kushukuru Mungu kila mara. Soma Wakolosayi 4:2 vilevile. Ingetupasa kushukuru Mungu siku zote kwa mambo yote, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo (Waefeso 5:20). Labda unafikili ni nguvu kushukuru Mungu kwa maneno fulani. Ni kweli, lakini hata hivi tunaagizwa kufanya hivi. Kumbuka ya kwamba Mungu anafanyiza maneno yote kuwa baraka kwetu (Waroma 8:28). Soma vilevile 1 Watesalonika 5:18 na tia mstari chini yake ndani ya Biblia yako.

Waandishi wa Zaburi walikuwa na sifa na shukrani mengi kwa Mungu. Ona Zaburi 26:7; 92:1; 95:1-2; 100:4. Usikose kusoma mashairi haya ndani ya Biblia yako.

Labda una majirani ambao walikuomba kuwasaidia ndani ya maneno fulani? Nawe ulitoa saa yako na kutumia mali yako kufanya hivi, lakini nyuma yake hawakuleta hata asante kwa masumbuko yako. Halafu ulifikili nini? Ungependa kuwasaidia tena? Siku moja Bwana Yesu alisafisha wakoma kumi. Alifikili nini wakati mmoja tu wa wakoma wale kumi aliporudi kumpa asante kwa sababu alimponyesha? Soma Luka 17:12-18. Basi Mungu anafikili nini wakati tunapoomba maneno karibu naye siku zote lakini hatumshukuru wakati anapojibu maombi yetu?

Mungu anataka sisi kuomba kwa sababu gani? Tunaona sababu moja hapa: ili tuweze kumsifu na kumshukuru wakati anapojibu maombi yetu. Tunamtukuza wakati tunapomtolea zabihu ya kushukuru (Zaburi 50:23).

Kwa sababu gani basi tutanyima Mungu mashukuru yetu? Ametupa Mwokozi wa ajabu (2 Wakorinto 9:15), na ndani ya Mwokozi huyu ametubariki na baraka zote za roho. Anatulinda

(1 Petro 5:7), na ameahidi kutupa sisi vitu vyote tunavyohitaji tungali hapa duniani (Matayo 6:25-33). Anaweka roho sana juu yetu (Matayo 10:29-31), na kutazamia siku wakati atakapotukaribisha kwake mbinguni kwa milele na milele (Yoane 14:1-2).

~ 19 ~

INANIPASA KUOMBA MARA NGAPI?

Kwa nini unauliza neno hili? Unaogopa ya kwamba Mungu atachoka na maombi yako?

Ni kweli ya kwamba zaidi ya watu wanachoka mbio wakati tunapoomba vitu karibu nao tena na tena, lakini Mungu ni namna nyingine na watu. Anafurahi sana kwa watoto wake kufika kwake na maombi kwa kila wakati. Nabii Danieli aliomba Bwana mara tatu kila siku (Danieli 6:10). Daudi alifanya vivyo hivyo (Zaburi 55:17).

Bwana Yesu alisema ya kwamba ingepasa watu kuomba siku zote (Luka 18:1). Katika 1 Watesalonika 5:17 tunaagizwa kuomba pasipo kuacha. Ni kusema ya kwamba kwa saa yo yote mchana au usiku unaweza na inakupasa kuomba Mungu kwa mahitaji yako mwenyewe na kwa mahitaji ya watu wengine vilevile.

~ 20 ~

INANIPASA KUOMBA MARA NGAPI KWA NENO FULANI MOJA?

Maandiko Matakatifu hayatupashi jibu la ulizo hili, lakini tunaagizwa kudumu katika maombi (Wakolosayi 4:2). Mtu mmoja wa jamaa yako hajaamini Kristo bado? Halafu ombea mtu huyu kila siku kufika wakati anapopokea Kristo kuwa Mwokozi wake. Labda itakupasa kuomba miaka mitano au kumi au zaidi.

Kuna neno fulani unalotaka sana na umeomba Mungu juu yake, lakini ni kama Mungu hakujibu? Kaa kuomba tu juu ya neno hili, lakini bila kusema na Mungu ya kwamba ni lazima kwake kujibu maombi yako na kufanya neno unaloomba kwake. Inakupasa kuomba namna Bwana Yesu alivyoomba katika shamba la Getesemane, "Si kama ninavyotaka mimi, lakini kama wewe unavyotaka" (Matayo 26:39). Labda neno unaloomba halipatani na mapenzi ya Mungu hata kama wewe ukifikili lingekuwa vizuri. Kwa mfano, labda una rafiki mmoja aliyetumikia Bwana sana sana kufika wakati aliposhikwa na ugonjwa. Sasa analala kitandani kwa majuma mengi na umeomba Bwana kumponyesha ili aweze kumtumikia tena. Lakini Mungu hamponyeshi. Kwa nini? Kwa sababu Mungu anayejua maneno yote anajua ya kwamba anaweza kufanya kazi hata kubwa kupita kwa njia ya rafiki yako pale kitandani, hivi anamwacha pale.

~ 21 ~

Mara nyingine Mungu anafanya neno ninaloomba kwake hata kama si mapenzi yake?

Ndiyo, anafanya hivi mara nyingine. Labda atafanya hivi kama ukimwambia ya kwamba ni lazima kwake kufanya neno unaloomba. Waza juu ya maneno mawili yaliyotokea kwa wakati wa Agano la Kale:

1. Bwana alikulisha Waisraeli na mana toka mbinguni wakati waliposafiri jangwani kwendea inchi ya Kanana. Waisraeli walianza kuchoka kula mana hii nyuma ya siku nyingi kidogo, hivi waliomba Mungu na nguvu kuwapa nyama bila kutafuta kufahamu kwanza kama neno hili ni mapenzi yake. Mungu aliwapa nyama kama walivyoomba lakini alituma ugonjwa mbaya sana katikati yao vilevile. Soma Zaburi 106:13-15 na Hesabu 11:4-9, 31-33. Unafikili ilikuwa vizuri kwa Waisraeli kuomba Mungu na nguvu kuwapa chakula kingine?

2. Mfalme Hezekia alikuwa mgonjwa sana na Bwana alituma nabii karibu naye kumwagiza kutengeneza maneno yake nyumbani kwa sababu kufa kwake kulikuwa karibu. Inaonekana wazi kwamba yalikuwa mapenzi ya Mungu kwa mfalme kufa kwa wakati ule. Lakini Hezekia hakukubali neno hili na aliomba Mungu sana sana aweze kumponyesha. Mungu alijibu maombi yake na alimwacha kuishi kwa miaka 15 mingine (2 Wafalme 20:1-6). Katika muda huu mwana wake Manase alizaliwa naye aligeuka mfalme wa Yuda nyuma ya kufa kwa baba yake. Hezekia alikuwa mfalme mzuri aliyeongoza watu wake kufuata Bwana lakini Manase alikuwa mmoja wa wafalme waovu zaidi wa Yuda, akaondosha watu wake karibu na Mungu na kuwafundisha kuabudu sanamu (2 Wafalme 21:1-3,16). Unafikili ilikuwa vizuri kwa Hezekia kuomba Mungu sana sana kumponyesha? Manase asingalizaliwa kama Hezekia angalikufa wakati Mungu alipokusudi kwaye kufa.

Mifano hii miwili inatufundisha ya kwamba haifai kwetu kuomba maneno na nguvu karibu na Mungu. Sharti tuombe ayafanye kama ni mapenzi yake tu. Umwambie Mungu maneno unayotaka ayafanye, lakini acha Mungu kuchagua kama atayafanya au sivyo.

~ 22 ~

INANIPASA KWENDA PAHALI FULANI KWA MAOMBI?

Hakuna agizo ndani ya Agano Jipya kusema sharti tuombe kwa pahali fulani tu, na tunaona ndani ya Biblia watu wakiomba kwa pahali mbalimbali:

Elia aliomba Mungu juu ya mlima Karmeli (1 Wafalme 18:36).

Hezekia aliomba Mungu kitandani (2 Wafalme 20:2).

Saulo aliomba Mungu wakati alipokuwa njiani kwenda Damasiki (Matendo 9:6).

Petro aliomba kwa dari ya nyumba pahali alipopanga (Matendo 10:9).

Paulo na Sila waliomba gerezani (Matendo 16:25).

Hata wewe ni pahali gani, ukifanya neno gani, unaweza na ingekupasa kuomba Bwana.

Ndani ya Waebrania 10:25 tunaagizwa vilevile kukusanyika na Wakristo wengine kuonyana na kusukumana katika mapendo. Bila shaka Wakristo waliomba pamoja kwa wakati ule vilevile. Kwa kufanya hivi tunaweza kukutana ndani ya nyumba ya Mungu au ndani ya nyumba ya ndugu Mkristo fulani, au pahali po pote pengine.

~ 23 ~

INANIPASA KUSHINDA SAA NGAPI KWA MAOMBI?

Hakuna jibu wazi ndani ya Maandiko Matakatifu kwa ulizo hili vilevile. Ni desturi nzuri sana, ndiyo desturi ya lazima kwa Mkristo kuweka saa fulani kila siku kwa kuomba Mungu peke yake. Ingempasa kusoma Neno la Mungu kwa wakati huu vilevile na kuacha Bwana kusemana naye kwa njia ya Neno lake. Saa nzuri zaidi kwa maneno haya ni asubui, mbele ya kuanza kazi ya nyumba (Zaburi 5:3). Saa hii Mkristo anapatishwa nguvu rohoni kushinda katika mambo na majaribu yote yatakayofika kwake kwa mchana ule.

Mara nyingine Mkristo atapenda kushinda saa tatu, ine au zaidi au hata mchana au usiku mzima katika maombi juu ya neno kubwa fulani. Kwa mfano labda unaomba Mungu kukujulisha nini anataka ufanye, au labda kuna matata fulani ndani ya kazi ya Bwana au maneno mengine yaliyo mazito rohoni mwako. Samweli aliomba Mungu usiku mzima (1 Samweli 15:11). Watumishi wengine wa Mungu wanashinda saa mbili au zaidi kwa maombi kila siku.

Mara nyingine tunaweza kuomba ombi fupi tu kwa sababu saa inakosa kwa ombi refu. Unakumbuka habari za Nehemia

wakati aliposimama mbele ya mfalme (Nehemia 2:1-8)? llikuwa kazi ya Nehemia kuangalia vinyweo vya mfalme na ilikuwa lazima kwake kuonekana na furaha kila mara alipotokea mbele ya mfalme. Lakini siku ile alikuwa na huzuni kwa sababu alikuwa amepokea habari za huzuni toka Yerusalema. Mfalme aliona huzuni yake, akamwuliza kwa sababu gani hakuwa na furaha. Halafu Nehemia aliomba Mungu mbio rohoni mwake, labda kwa nusu ya dakika tu angali alikuwa akisimama mbele ya mfalme (sh.4). Bila shaka aliomba Mungu kumpa akili aweze kujibu mfalme vizuri. Kisha aliomba mfalme kumruhusu kurudi kwa inchi ya Yuda kusudi ajengishe tena ukuta wa Yerusalema, na mfalme alikubali.

Neno kubwa si kama tukishinda dakika ngapi au saa ngapi kwa maombi, lakini ni kwa roho zetu kushinda na hali ya maombi wakati wote. Kama ni hivi, itageuka desturi kwasi kuomba Mungu mara nyingi kwa mchana mmoja hata wakati tunapofanya maneno mengine. Kwa njia hii tutakuwa na upatano wa karibu, ushirika mtamu sana na Bwana wetu wakati wote.

~ 24 ~

INANIPASA KUKAA NAMNA GANI SAA NINAPOOMBA?

Hakuna agizo ndani ya Biblia kusema sharti tusimame au kuketi au kupiga magoti au kukaa namna yo yote wakati tunapoomba.

Kwa wakati wa Agano la Kale wengine walilala kifudifudi udongoni wakati walipoomba, kama Musa na Haruni (Hesabu 16:22), na Yosua (Yosua 5:14). Elia aliinama na kuweka uso wake katikati ya magoti yake (1 Wafalme 18:42). Watu wengine waliinamisha vichwa vyao kama mtumishi wa Abrahamu alivyofanya (Mwanzo 24:26); na Waisraeli (Kutoka 4:31; 12:27); na Musa (Kutoka 34:8). Wengine walipiga magoti, kama Solomono (1 Wafalme 8:54; 2 Mambo 6:13), na Ezra (Ezra 9:5), na Danieli (Danieli 6:10).

~ 25 ~

Ni kama watu walisimama kwa maombi wakati Bwana Yesu alipokuwa duniani (ona Marko 11:25). Mfarisayo na mtoza kodi walisimama wakati walipoomba (Luka 18:10-13). Stefano alipiga magoti wakati alipoomba Mungu kusamehe Wayuda waliokuwa wakimwua kwa njia ya kumtupia mawe (Matendo 7:60). Petro alipiga magoti wakati alipoomba Mungu kufufua Dorika (Matendo 9:40). Paulo alipiga magoti wakati alipoomba pamoja na wazee wa Efeso (Matendo 20:36).

Kwa wakati wa sasa zaidi ya watu wana desturi ya kupiga magoti wakati wanapoomba Mungu peke yao. Wengine wanafanya vivyo hivyo wakati wanapokutana na watu wengine kwa maombi. Ndani ya makusanyiko mengi ya maombi mtu mmoja anasimama na kuongoza wengine kwa maombi nao wanasimama au kuketi wakiinamisha vichwa vyao. Watu wengi wanafunga macho yao wakati wanapoomba ili maneno ambayo yanawazunguka yasiondoshe mawazo yao kwa maombi.

Hivi tunaona ya kwamba wengine wa watu ambao tunasoma habari zao ndani ya Biblia waliomba wakisimama, wengine walipiga magoti, wengine walilala kifudifudi udongoni. Neno kubwa si kama tukisimama au kupiga magoti au kulala kifudifudi saa tunapoomba, lakini kama tukiwa na roho ya kunyenyekea mbele ya Mungu. Ingetupasa kuomba na roho ya unyenyekevu, tukikumbuka ya kwamba Mungu hana deni kwetu. Hatustahili kupokea hata moja ya baraka zake zote; tunaweza kumkaribia kwa njia ya maombi kwa sababu ya neema yake tu.

Kwa wakati wa kuja viumbe vyote mbinguni, duniani, na chini ya dunia watapiga magoti mbele ya Kristo na kutangaza wazi ya kwamba yeye ndiye Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba (Wafilipi 2:10-11).

~ 26 ~

Ni vizuri kwa mimi kuomba wakati mimi ni peke yangu tu, au pamoja na watu wengine vilevile?

Umejifunza mbele ya kwamba ni sharti kwa Mkristo kuomba peke yake kila siku. Ona ukurasa 25 na kuusoma tena.

Ulisoma vilevile ya kwamba tunapaswa kukusanyika pamoja na Wakristo wengine kwa kusukumana katika mapendo na kazi nzuri (Waebrania 10:24-25). Tunafanya hivi kwa njia ya kusoma Neno la Mungu na kuomba na kusifu Mungu pamoja (Waefeso 5:19-20; Wakolosayi 3:16). Mungu ametupa sisi agizo hili kwa sababu anajua ushirika pamoja na Wakristo wengine utatusaidia. Bila maneno haya roho zetu zinapoa mbio mbio.

Waamini walianza kukutana pamoja kwa maombi mara moja nyuma ya kurudi kwa Bwana Yesu Kristo mbinguni (Matendo 1:14). Kisha karibu watu 3000 waliamini siku ya Pentekote. Watu hawa walikutana pamoja kwa maombi (Matendo 2:41-42). Katika Matendo 12:5,12 tunaona ya kwamba Wakristo wengi walikuwa wamekutana nyumbani mwa Maria kuombea Petro aliyekuwa gerezani kwa wakati ule. Naye alifunguliwa.

Kuna ahadi nzuri sana kwa hata watu wawili wanaopatana kuomba juu ya neno fulani. Yesu alisema neno hili litafanywa na Baba yake mbinguni (Matayo 18:19)!

~ 27 ~

INAPASA MTU KUOMBA NAMNA GANI KATIKA KUSANYIKO LA WAKRISTO?

Katika makusanyiko ya Wakristo mtu mmoja anasimama kuongoza watu wote walio pale kwa maombi. Wakati anapomaliza, mtu mwingine anasimama na kufanya vivyo. Ingepasa watu hawa kusema na sauti ya nguvu kidogo ili watu wote

waweze kuwasikia. Vizuri waombe kwa mambo yale yaliyo mzigo wa Wakristo wote pale, si kwa mahitaji yao wenyewe.

Sharti wale wanaoongoza watu wengine kwa maombi wataje maneno fulani mbele ya Mungu. Haifai waombe, "Bwana, bariki watumishi wako wote pahali pote duniani," lakini "Bwana, bariki ndugu zetu fulani waliokwenda kuhubiri Habari Njema yako kwa kijiji fulani." Sharti wamwambie Mungu nini wanayotaka afanye kwa ndugu hawa, wakitaja namna ya kazi yao na mahitaji na masumbuko yao yote mbele yake. Mungu anataka sisi kumwambia wazi nini tunayotaka atufanyie kama ikipatana na mapenzi yake. Halafu wakati Bwana anapojibu maombi yetu tunafahamu kwamba anajibu maombi fulani. Neno hili litatusukuma kumsifu na kumshukuru, na litatupa hamu kudumu katika maombi.

Kuna maneno mawili ambayo inakupasa kuepuka wakati unapoongoza watu wengine katika maombi:

1. Usiongoze watu kwa maombi kusudi uonekane kama Mkristo mzuri mbele yao! Ona Matayo 6:5.
2. Usiombe maombi marefu marefu ya masemo mengi. Bila shaka wengine ndani ya kusanyiko lenu la maombi wana mzigo rohoni vilevile juu ya maneno mengine wanayotaka kuyaleta mbele ya Bwana. Kwa sababu hii si vizuri kwa mtu mmoja au watu wawili kumaliza saa nzima iliyowekwa kwa maombi.

~ 28 ~

MAOMBI YATAGEUZA MAISHA YANGU KWA NJIA YO YOTE?

Ndiyo. Waza juu ya maneno haya matatu:

1. **Maombi yatakupa FURAHA**. Bwana Yesu alisema, "Mwombe, na mutapata, furaha yenu itimizwe" (Yoane 16:24). Utafurahi sana kuona Bwana akifanya maneno yale ambayo

ulimwomba kufanya kwa sababu utafahamu ya kwamba yeye ni karibu sana nawe na anakufikili pamoja na maneno yako yote. Ni kusema wewe na Bwana wako muna upatano mtamu sana.

2. **Utapata NGUVU mpya** kwa njia ya kungojea Bwana kwa maombi (Isaya 40:31), ndiyo nguvu ya roho kushinda majaribu na kudumu katika kazi ya Bwana hata wakati wa matata na mazuizo. Mara nyingine Bwana ataongeza hata nguvu yako ya mwili kama ukihitaji nguvu kubwa kupita kumtukuza yeye.

3. **SALAMA ya Mungu itajaza roho yako** kama unaweka mahitaji na mafazaiko yote mikononi mwa Bwana kwa sababu unajua Bwana Yesu ataangalia maneno haya yote na kutengeneza yote kwa baraka yako. Soma Wafilipi 4:6-7.

~ 29 ~

MAOMBI YANA FAIDA GANI KWA KAZI YA BWANA?

Maombi ya watu wa Mungu yanafanya kazi nyingi kusaidia Habari Njema kuendelea mbele kwa sababu kuna uwezo na baraka ndani ya maombi (Yakobo 5:16). Tunaweza kuona neno hili katika maisha ya Elia wakati Bwana alipojibu maombi yake na kufufua kijana aliyekufa (1 Wafalme 17:21-22). Mbele ya wakati ule Elia aliomba Mungu kuzuiza mvua isinyeshe. Alitaka kuonyeshea watu wa Yuda ya kwamba Mungu aliwakasirikia kwa sababu ya zambi zao. Bwana alijibu maombi ya Elia na mvua haikunyesha kwa miaka mitatu na nusu (Yakobo 5:17). Halafu wakati watu waliporudi karibu na Mungu Elia aliomba Mungu kutuma mvua tena na mvua ilianza kunyesha (1 Wafalme 18:41-46).

Wakristo kwa wakati wa mwanzo wa Kanisa waliomba Bwana kuwapa uhodari kumshuhudia wakati adui zao walipo-

jaribu sana kuwaogopesha. Mungu alijibu maombi yao? Ona Matendo 4:29-31.

Hakuna neno Mungu asiloweza kufanya kwa kujibu maombi ya wale wanaokaa ndani ya Kristo (Yoane 15:7). Watu hawa wanaomba tu kwa maneno yale yanayopatana na mapenzi ya Mungu kwa sababu mawazo yao yanaongozwa na Neno lake, hivi Mungu anaweza kufanya maneno wanayoomba kwake.

Unataka Mungu kufanya nini ndani ya maisha yako mwenyewe na kazi yako kwaye? Unataka afanye nini ndani ya maisha na kazi ya watu wengine? Kuna pahali pengine duniani Habari Njema isipoweza kuingia nawe ungependa sana watu wa pahali pale waweze kuisikia vilevile? Kuna watu wengine ambao uliwafudisha juu ya njia ya wokovu tena na tena lakini mioyo yao ni migumu kama mawe? Mungu atafanya maneno yasiyowezekana kwa watu kwa sababu ya maombi yako kwani kuna uwezo kwa maombi. Tumika na uwezo huu kwa utukufu wake na utabarikiwa zaidi.

~ 30 ~

NAMNA GANI NINAWEZA KUJIFUNZA KUOMBA?

Unauliza vizuri. Wanafunzi waliomba Bwana Yesu kuwafundisha kuomba. Alifanya hivi kwa njia ya kuwapa mfano wa maombi tuliosoma katika Luka 11:1-4. Tuliwaza juu ya mfano huu mbele.

Halafu fikili juu ya mtoto na baba yake. Inapasa mtoto kujifunza namna gani kuomba baba yake kwa kitu fulani? Sivyo, hahitaji mtu kumfundisha namna gani kuomba kupewa kitu anachotaka. Anasema tu, “Baba, tafazali unipe maji nipate kunywa.”

Halafu kumbuka ya kwamba Mungu ni Baba yako ya mbinguni. Unahitaji kweli kujifunza namna gani kuomba Baba yako ya mbinguni kwa mahitaji yako? Labda hujui kusema maombi yako na maneno marefu mazuri mazuri, lakini neno hili si kitu kwa Mungu. Anakusikia hata hujui kusema vizuri kwa sababu wewe ni mtoto wake naye anakupenda. Anajua roho yako yote.

Kuna maneno mengi tunayojifunza kwa njia ya kujaribu kuyafanya, kama kutembea, kusema, kusoma, na mengine. Ni vivyo hivyo na maombi. Kwa kipimo unachoomba, kwa kipimo hiki utajua namna gani kuomba. Mungu atupe sisi sote hamu kubwa kugeuka mafundi kwa maombi!